

## **MAZOEZI WAKATI WA LIKIZO**

### **KIDATO CHA TATU**

#### **EDK**

1. (a) Elezea kwa kifupi hali ya amani ilivyokua kwa waislamu wakati wanaanzisha dola na uchache wao katika usalama wao.  
(b) Eleza kwa kifupi njia kuu nne alizotumia mtume saw kama kiongozi wa dola ya kiislamu kujilinda kiusalama.  
(c) Je ruhusa ya kupigana kwa mwislamu imetolewa katika misingi gani ?  
(d) Taja sababu nyingi zinazomlazimisha mwislamu kuingia katika mapigano.  
(e) Ni zipi faida za mapigano au Jihaad katika uislamu.
2. Unafiki ni ugonjwa uliopelekea kuyumba kwa dola ya kiislamu wakati wa mtume saw, lakini Allah SWT akamwamuru Mtume wake saw hatua za kuchukua kukabiliana na wanafiki, Taja hatua kuu tatu alizoamrisha mtume achukue dhidi ya wanafiki ili kuwamaliza kabisa kwa ushahidi wa Qurani.
3. (a) Vipi uislamu umesema kuhusu amani na utulivu ?  
(b) Taja maonyo yaliyoletwa na Qurani juu ya jambo la Amani na kuidumisha.  
(c) Ipi hokum ya mchafua amani au mchochezi wa kuvunja Amani wakati ipo misingi ya amani ?  
(d) Ni ipi misingi inayoletwa na Amani (matunda ya Amani) ?
4. Ni yapi madhumuni makuu ya dola ya kiislamu ?
5. Mtume saw alianzisha mfumo imara wa mapato na matumizi (revenue system) elezea kwa ufupi njia sita alizotumia mtume saw kama njia ya mapato katika serikali ya kiislamu.
6. Elezea misingi minane ya katiba ya kiislamu katika dola ya kiislamu.
7. (a) Orodhesha makundi matano yaliyokuwa maadui wa dola ya kiislamu wakati wa mtume saw.  
(b) Eleza sababu za vita vya badri, kutokea kwake ,mafunzo yake kwa waislamu wa leo.

TAFADHALI ANDIKA NA JIBU MASWALI HAYA KATIKA DAFTARI